# Biblia inasemaje kuhusu Pombe?

"Mtu akienda kwa roho ya uongo, akinena maneno ya uongo, akisema, Nitakutabiria habari ya mvinyo na kileo; mtu huyu atakuwa nabii wao watu hawa!" Mika 2:11.

Umewahi kuwasikia watu wanapohaha namna ya kuhalalisha unywaji pombe kwa kusema, "Biblia haisemi Usinywe Pombe?"

Hivi,kwanini siku hizi watu wanataka kuwa wema tu? Kuwa msamaria mwema tu? Hivi ni kwa nini wengi hupenda kujiingiza katika hali zisizo bora? Siku hizi sisi wakristo lazima tutambue kwamba kuwa mwema si bora. Na lazima tuwe tayari kujitahidi kuwa bora kwa ajili ya Bwana. Kama vile jana nilivyosikia katika hotuba, "kuwa mwema huififisha haki yetu ya ubora." Na wakolosai 1:18 yafundisha, Yesu ni mtangulizi katika yote.

Nakumbushwa juu ya simulizi inayowahusu Mariamu na Martha katika Luka 10:38-42. Martha alikuwa anahangaika ili kuwahudumia wageni wake wote, jambo ambalo ni jema. Walakini, Martha alipomtaka Yesu amkaripie Mariamu kwa sababu ya kutomsaidia kuwahudumia wageni, badala yake Yesu alimkaripia Martha kwa kufanya lililo jema. Alimkaripia Martha kwa sababu Mariamu alikuwa anafanya jambo bora. Alikuwa anamsikiliza Yesu. La msingi ni kwamba, katika kila hali kunakuwapo jema na bora. Je, unadhani Yesu anapendelea nini kutoka kwetu linapokuja suala la pombe? Najua wengine hudhani ni njema, lakini, hivi kweli pombe ni bora?

Kwanza, "Yesu alitengeneza divai ili kuhalalisha unywaji pombe?". Sote tumepata kusikia hoja hii kutoka kwa walimwengu. Natambua wenye dhambi hujaribu kuhalalisha hamu yao ya pombe. Hakuna anayetaka kuitwa mpotofu. Hata ingawa hoja hii inanikera, hainikeri kwa kiwango kikubwa kama ninapomwona mkristo anaanza kutumia hoja hii hii ya kale iliyochakaa.

Naam, Naam, Naam, Yohana 2:1-11 panasema Yesu alitengeneza divai.

1. Tunatakiwa kulielewa vizuri jabo hili, kwani kama Yesu alimpa pombe mkuu wa meza ili wanywe, basi Yesu alitenda dhambi!!!! Habakuki 2:15 yasema "Ole wake yeye ampaye jirani yake kileo"
2. Neno la Kiyunani lililotumika kuzungumzia divai katika Biblia ni neno la kiujumla, laweza kumaanisha divai au mvinyo ilevyayo. Na tunaacha fungu hili la maandiko liamue ni aina gani ya kinywaji kilichokuwa kinaongelewa. Isaya 16:10 "Akanyagaye hakanyagi divai katika mashinikizo; nimeikomesha sauti ya furaha yake akanyagaye". Sasa kwenye mashinikizo kunatoka nini? Inatoka mvinyo au divai? Na bado Biblia ya kiingereza imetafsiri kuwa kinachotoka kwenye shinikizo kuwa mvinyo (wine). Wakati huo huo twajua ya kuwa maji yanayokamuliwa kutoka kwenye zabibu ni divai. Ushahidi ni hapa jinsi neno hili lilivyotumika kiujumla, limeingizwa katika lugha ya Kiingereza kama mvinyo, na lazima tuache fungu la maandiko kuamua kama kinachokusudiwa ni mvinyo au divai. Unaweza kuona hali hiyo hiyo katika Yoeli 2:24

Pili, tena nimewahi kusikia hoja kwamba "Mungu hakusema usinywe pombe."

1. Mtazamo huu juu ya Biblia ni potofu. Biblia inatufundisha “Kwa maana tunda la nuru ni katika wema wote na haki na kweli; {Kumbuka kweli imefunuliwa wapi? Roho Mtakatifu}. Mkihakiki ni nini impendezayo Bwana. Wala msishirikiane na matendo yesiyozaa ya giza, bali myakemee; kwa kuwa yanayotendeka kwao kwa siri, ni aibu hata kuyanena,” Waefeso 5:9-12. Namna sahihi ni “hakiki ni nini impendezayo Bwana”. Kiukweli, si kazi yangu kukosoa na silazimiki kukuonyesha kwamba unywaji pombe ni kosa. Mbinu ya kutumia inapaswa kuwa, kwenye pombe kuna ubora gani? Kwenye unywaji pombe kuna ubora gani? Sisi kama wakristo, tunatakiwa kutia muhuri wa kukubali juu ya mambo yenye ubora. “Mpate kuyakubali yaliyo mema; ili mpate kuwa na mioyo safi; bila kosa, mpaka siku ya Kristo.” Wafilipi 1:10

   Halafu tena, hivi Mungu hajawahi kumwambia mwanadamu “Usinywe kileo?” Um, Walawi 10:9, “Usinywe divai wala kileo chochote.” Mstari huu waliandikiwa makuhani. Hivi sisi siyo makuhani? “ Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme….” 1 Petro 2:9. Hesabu 6:3 panaeleza kwamba waliokuwa wanadhiri hawakuruhusiwa kunywa vileo. Katika Kumbukumbu 29:6 Wana wa Israeli walijiepusha na vileo ili kwamba wapate kushika maarifa sahihi ya Mungu. Katika Mithali 20:1 mwenye hekima aliandika “Mvinyo hudhihaki, kileo huleta ugomvi. Na akosaye katika vitu hivyo hana hekima.”

   Mithali 31:4 Panasema kwamba kunywa mvinyo hakuwafai wafalme na wakuu. Tena, Wana wa Mungu si wafalme na wakuu? Ufunuo 1:6? Isaya 24:9 panasema, “hawatakunywa divai pamoja na nyimbo.” Isaya 28:7 yasema “ Hawa nao wamekosa kwa divai; wamepotea kwa kileo.”

2. Biblia inatufundisha kwelikweli kwamba tusinywe pombe. Nadhani swali linalobaki ni kwamba, tuko tayari kumpa Mungu yaliyo bora?yenye ubora naya kwanza? Hivi ni lini unywaji pombe ukawa ndiyo jambo bora la kumpa Mungu?

Najua kwamba yapo mafungu mengi katika Agano la Kale na Agano ambayo tungetakiwa kuyaangalia. Kuna hoja nyingi nzito na muhimu ambazo zingejitokeza. Lakini mtu **anayejitahidi kwa kadri awezavyo kwa ajili ya Mungu** ataona dhahiri ambacho mafungu haya yanafundisha. 1) Yesu asingetengeneza pombe na kumpa mwanadamu. Kufanya hivyo kungekuwa ni uvunjifu wa wazi kabisa wa Habakuki 2:15. 2) Mungu anasema, “Msinywe divai, wala kileo.” 3) Mungu anajua kuwa watu watataka kunywa pombe hadi watafikia hatua ya kutafuta waalimu wa uongo,ambao Mungu anawaita “wadanganyifu” ili wawambie kuwa ni halali kunywa vileo, Mika 2:11

Na kwa kuhitimisha nawasihi tutafakari Mika 2:11. Hapa Mungu anaelezea “furushi la uongo livumalo” na jinsi watoto wake waliopotoka walivyowapenda wahubiri wa namna hii. Mika anasema “mtu akienda kwa roho ya uongo , akinena maneno ya uongo, akisema, nitakutabiria habari ya mvinyo na kileo; mtu huyu atakuwa nabii wao watu hawa.” Maana ya Mungu iko wazi katika mistari ya 7-11. Yaani, wasioipenda kweli watampenda na kumfuata haraka mtu anayesema ni halali kunywa pombe. Paulo alisema hivyo hivyo katika 2 Timotheo 4:3 “Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye

uzima; ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe wataipatia waalimu makindi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti.” Lakini kumbuka, Mungu anasema mwalimu huyo “anadanganya,” Mika 2:11